

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
24 Novemba 2007**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Husein Hamza Hamisi
Izdoly Aludo Kihalule
Juma Ali Salehe Jongo
Kassim Bakari
Paulo Atibu Hatibu
Rahma Ali
Sudi Saidi Ramadhan

Siku ya uamsho wa mabadaliko ya majira

Sosthenes alipewa hela ya kutengeza mabango kwa ajili ya siku ya uamsho wa mabadaliko ya majira na ameshatengeneza lakini hakuweza kuhudhuria mkutano.

Elaine alimtembelea Bwana Manyika wa Ofisi ya Makamu Rais. Yeye na katibu mkuu na wengine wanaenda jiji la Bali, Indonesia kwa ajili ya mazungumzo ya mabadaliko ya majira, basi hawatakuwepo tarehe 8 Desemba. Alipenda sana mpango wetu na alisema tuandike barua ya kuomba watu wa kutupokea tarehe 8 Desemba. Juma alimletea barua hii ijumaa.

Ubalozi wa Merekani walikuwa na siku kuu alhamisi na hatujawasiliana nao bado.

Damas alimtumia kwa email kwa Elaine orodha ya mashirika ya mazingira na namba za simu na anwani za email na alijaribu kutafuta ofisi zao zipo wapi. Juma na Filbert walisema watazunguka ofisi hizi kusanya saina wiki hii. Elaine alisema ataandika kurasa ya taarifa kueleza kwa mashirika kuhusu tukio na malengo yake.

Juma alipendekeza tuwape taarifa kwa CHABADA ili washirikiane.

Msafara wa Baisikeli

Ubalozi wa Uholonzi waliomba tusahihisha repoti yetu kidogo na Elaine alisahihisha na sasa wanajiandaa kulipa hela ya udhamini unayobaki.

Ofisi, guta na mambo ya hela

Bao mpya za tangazo bado zinatengenezwa.

Violeth alimpa dondoo za kiswahili kwa Elaine lakini bado lazima Elaine azitengeneze ili kuziprintia.

Spea za guta bado hazijafika.

Wamba memorial fund walijibu na bado hawajafanya uamuzi kuhusu udhamini wa mradi wa usalama barabarani, na watatupa taarifa watakapofanya uamuzi.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji

Bwana Wemba bado hajajibu barua yetu ya kuomba semina ya usalama barabarani.

Halmashauri ya Jiji

Ally Saidi Mohammed hakuwepo kwenye mkutano basi hatukuweza kutengenza maoni kuhusu barabara ya Morogoro. Juma alifuatalika na halmashauri ya jiji kuhusu barua yetu na Mama Mlamba alisema tutapata jibu kwa posta.

Nyingenezo

Tuliamua tutamaliza mikutano saa sita mchana ili wanachama wanaweza kupanga ratibu zao zingine za kila jumamosi.